JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

**S.L.P. 38 KYAKA - KAGERA**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KGR/MSY/J.1/18/VOL.II/1 **2/04/2024**

**KWA WANANCHI WOTE**

c/o Watendaji wa Kata Zote,

**Halmashauri ya Wilaya Missenyi.**

# TANGAZO

**YAH: KUTOA MAONI YA SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA MWAKA 2024 ZA HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI**

Rejea mada tajwa hapo juu,

2. Halmashauri imedhamiria kutunga Sheria Ndogo za Ada na Ushuru (Marekebisho), 2024. Katika utungwaji wa sheria ndogo hizi, Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Sura 287 R.E 2002 Kifungu cha 153 kinahitaji maoni/mapendekezo ya wananchi yatolewe ili Baraza la Madiwani na Waziri Mwenye Dhamana waweze kufikia maamuzi sahihi ambayo yanaendana na matakwa ya wananchi katika utungwaji wa sheria ndogo hizo. Kutokana na hali hiyo, nakutumia Tangazo hili pamoja na nakala ya sheria ndogo inayopendekezwa ili zibandikwe kwenye mbao za Matangazo kwa ajili ya wananchi kuziona na kutoa mapendekezo /maoni.

3. Aidha, mbali na maoni ya mtu mmoja mmoja au taasisi, ninawaelekeza kuitisha kikao cha WDC ili kujadili sheria ndogo hizi na kuleta maoni ndani ya siku 14 tokea tarehe ya kutolewa tangazo hili.

4. Ninaomba mapendekezo hayo yawasilishwe ndani ya muda uliopangwa ili sheria ndogo hizo ziweze kujadiliwa na baraza la Madiwani ndani ya robo hii.

5. Kwa yeyote ambaye atakwama au kutaka ufafanuzi zaidi, awasiliane na Mwanasheria wa Halmashauri kwa simu namba 0755420290/07666666691.

6. Maoni hayo yawasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji moja kwa moja au kupitia anwani tajwa hapo juu mnamo au kabla ya tarehe 15/04/2024.

7. Nawatakieni utekelezaji mwema ndani ya muda ulioainishwa.

Mwl. Warento N. Warento
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI

**Nakala**:

: Mbao za matangazo

: Katibu Tawala (W)

S.L.P 38 Kyaka, Simu: +255 28 298 2836, Nukushi: +255 28 298 2834, Barua pepe: ded@missenyidc.go.tz,
Tovuti: www.missenyidc.go.tz

`TANGAZO LA SERIKALI NA ..................... la tarehe ............................

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu 7(1) na 16(1)*

**SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI, 2024.**

| | |
|---|---|
| Jina | 1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi (Marekebisho), 2024 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, 2020. |
| GN.No. 671 /2020 | |
| Tarehe ya kuanza kutumika | 2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kuanzia tarehe ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Marekebisho ya Jedwali la Kwanza | 3. Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo Kuu Kipengele AI(1)- (7) cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo; |

A. USHURU WA MAEGESHO

I. Ushuru wa maegesho ya mitumbwi

1. Mitumbwi .................... 50,000/- kwa mwaka

2. Kalua/Ngama ............... 50,000/- kwa mwaka

3. Kivuko 'Ferry'.............. 50,000/- kwa mwaka

4. Meli Ndogo .................. 50,000/- kwa mwaka

5. Boti iliyobeba sanduku za kubeba samaki .......50,000/- kwa mwaka

6. Makontena .................. 50, 000/- kwa mwaka

7. Mitumbwi ya kusafirisha abiria ............................ 50,000/- kwa mwaka

4. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu Kipengele BII(5) cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo:

B. USHURU WA MAZAO YA MAJINI

II. Bidhaa za majini

5. Mabondo ........................ 6,000/- kwa kilo

5. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele BII kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 8 kitakavyosomeka kama ifuatavyo:

**B.** USHURU WA MAZAO YA MAJINI

II. Bidhaa za majini

8. Vyambo .....1,000/- kwa dumu la lita 20

6. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipenge cha C11 kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo;

C. USHURU NDANI YA MASOKO NA MAGULIO KWA SIKU

11. Mazao ya kilimo kwa gunia/tenga...... 1,000/-

7. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo kipengele cha D1, D(2), D(4), (D5) na D(9) kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo:-

D. USHURU WA MAZAO YA MISITU

1. Gunia la mkaa ...........2,000/-

2. Mbao ..... 300/- kila ubao usiozidi futi 12 za 1x8,1x10,2x3,2x6

- 300/- kila ubao wenye vipimo vya 2x2,1x4

3.kwa urefu usiozidi futi 12 ................ 300/- (kila futi itakayoongezeka 50/-)

4. Nguzo .................... Tsh. 500/- (kipenyo cha sentimita 11-20 )

5. Gogo ....................... Tsh. 2,000/- (kipenyo cha sentimita 21 na kuendelea)

9. Kibali cha kukata mti na kuvuna mti ..... 500/- kila mti (zamani 1,000/-)

8. Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele cha D kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 12 kitakavyosomeka kama ifuatavyo:

D. USHURU WA MAZAO YA MISITU

12. Papara ................. Tsh. 200 kila papara wenye vipimo vya 1x4

9. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele EI cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo;

**E.I ADA YA VIBALI VYA UTAMADUNI**

1. Kibali cha sherehe/hafla katika maeneo ya miji ya Mtukula, Bunazi, Kyaka ...100,000/- kwa tukio

2. Kibali cha sherehe katika maeneo ya mengine ...................50,000/- kwa tukio

10. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele cha EI kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 3,4 kitakavyosomeka kama ifuatavyo;

3. Ukodishaji wa matenti (1-5).......... 20,000/- kwa tukio

4. Ukodishaji wa matenti (5-10) ....... 50,000/- kwa tukio

11. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele G(3)(G2) cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo;

**G. ADA YA VIBALI VYA UJENZI**

3. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya jengo la biashara...........600/=kwa M2

4. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya kituo cha mafuta ........... 1,500/= kwa M2

12. Jedwali la Sheria Ndogo Kuu kipengele cha G kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 4 kitakavyosomeka kama ifuatavyo;

G. ADA YA VIBALI VYA UJENZI

4. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya jengo la Godown ........ 1,000/- kwa M2

13. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele cha H kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 13 kitakavyosomeka kama ifuatavyo:

**H. ADA YA UKAGUZI WA AFYA**

13. Godauns/stoo .................................20,000/- kila baada ya miezi 6

14. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele J kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 8, 9, 10, 11 na 12 kitakavyosomeka kama ifuatavyo:

**J. ADA NA USHURU WA ARDHI**

(8). Maombi ya hati ya kimila Tsh. 20,000/-

(9). Maombi ya kupanga na kupima Ardhi Tsh. 20,000/-

(10). Maombi ya kufufua/kurudisha mipaka Tsh. 50,000/-

(11) Ukaguzi michoro ya mipango miji Tsh. 100,000/-

(12) Usajili hati kimila 1% ya thamani ya ardhi

10. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu Kipengele J(5) na J(7) cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo:

**J. ADA NA USHURU WA ARDHI**

J(5). Maombi ya kuhakiki hati miliki.... 40,000/- $M^2$

J(7). Ada ya uuzaji ardhi ambayo haijapimwa 5% ya bei ya soko au mkataba wa mauziano

15. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu Kipengele K(8),(9),(10),(13) na K(14) cha Sheria Ndogo Kuu kinafutwa na badala yake kusomeka kama ifuatavyo:

**K. USHURU MWINGINE**

8. Gari lenye maganda ya kahawa 1-2.5 $M^3$ .....10,000/-kwa safari

9. Gari lenye maganda ya kahawa 2.5- 6.7 $M^3$ ......80,000/- kwa safari

10. Gari lenye maganda ya kahawa 6.7 $M^3$ na kuendelea......100,000/- kwa safari

13. Kupakia au kupakua bidhaa za viwandani gari lenye 1-2.5 $M^3$ ...........20,000/- kwa safari

14. Kupakia na kupakua bidhaa za viwandani gari lenye 2.5-6.7 $M^3$ ..........50,000/- kwa safari

16. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 18,19,20,21,22,23 kitakavyosomeka kama ifuatavyo:

**K. USHURU MWINGINE**

18. Kupakia na kupakua bidhaa za viwandani gari lenye 7.3 $M^3$ na kuendelea........100,000/- kwa safari

19. Gari la kusafirisha chuma chakavu 1-2.5 $M^3$ .....................10,000/- kwa safari

20. Gari la kusafirisha chuma chakavu 2.5-6.7 $M^3$ .....................50,000/- kwa safari

21. Gari la kusafirisha chuma chakavu 7.3 $M^3$ na kuendelea ........100,000/- kwa safari

22. Usajili wa mitego ya kuvuna senene Mitego 1-5......... -50,000/- kwa mwaka

23. Usajili wa mitego ya kuvuna senene Mitego 6 na kuendelea.....100,000/- kwa mwaka

17. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo Kuu kipengele L kinarekebishwa kwa kuongezewa kipengele kidogo cha 4,5,6 kitakavyosomeka kama ifuatavyo:

**L. ADA MBALIMBALI**

4. Ada ya usajili wa bajaji ya biashara ndani ya Halmashauri............30,000/- kwa mwaka

5. Ada ya usajili wa pikipiki biashara...........10,000/-kwa mwaka

6. Ada ya usajili wa tax ya biashara ......... 40,000/- kwa Mwaka

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi kilichofanyika tarehe ……………… na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya-

………………

***PROJESTUS K. TEGAMAISHO***
Mwenyekiti Halmashauri Ya Wilaya ya Missenyi

…………………

***J OHN P. WANGA***
Mkurugenzi Wa Halmashauri ya Wilaya Ya Missenyi

NAKUBALI,

……………………..

Waziri wa Nchi
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**DODOMA**

Tarehe ……………………………………..